**MTIHANI WA PAMOJA WA KASSU, JUNI-JULAI 2022**
Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari
KISWAHILI
Karatasi ya 1
INSHA
Saa 1 ¾

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**
**(SIRI)**

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com

1. **LAZIMA.**
   Chamko la ugonjwa wa Korona lililemaza shughuli za michezo nchini. Wewe ni katibu wa jopokazi lililoteuliwa na Waziri wa Michezo kubuni mikakati ya kufufua michezo katika taasisi za elimu nchini. Andika kumbukumbu za mkutano huo.

2. Vijana wamekuwa wakichelea kuhusika katika mchakato wa uchaguzi. Jadili vyanzo vya hali hii huku ukiwapendekezea vijana umuhimu wa kubadili msimamo huu.

3. Tunga Kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo: Achanikaye kwenye mpini hafi njaa.

4. Andika insha itakayomalizikia kwa …nilipotua nchini, nilishusha pumzi, nikamshukuru Jalia kwa kuponea chupuchupu katika uvamizi huo.

1. **LAZIMA.**
   **Chamko la ugonjwa wa Korona lililemaza shughuli za michezo nchini. Wewe ni katibu wa jopokazi lililoteuliwa na Waziri wa Michezo kubuni mikakati ya kufufua michezo katika taasisi za elimu nchini. Andika kumbukumbu za mkutano huo.**

Hii ni insha ya kumbukiumbu. Utaini wake ujikite katika vipengele viwili vikuu:

a) Muundo
b) Maudhui

**a) Muundo**

i) Kichwa kionyeshe:

a) Kundi linalokutana
b) Mahali pa mkutano
c) Tarehe ya mkutano
d) Wakati wa mkutano

ii) Waliohudhuria-vyeo na nyadhifa zao zidhihirishwe
iii) Waliokosa kuhudhuria kwa udhuru
iv) Waliokosa kuhudhurria bila udhuru
v) Waalikwa/Katika mahudhurio- hawa ni wale waliohudhuria mkutano japo si wanachama ( si lazima)
vi) Ajenda za mkutano
vii) Kumbukumbu zenyewe/ kiini cha mkutano:

a) Utangulizi/ kufunguliwa kwa mkutano
b) Wasilisho la mwenyekiti
c) Kusomwa na kuthibitishwa kwa kumbukumbu za mkutano uliopita/uliotangulia
d) Yaliyoibuka kutokana na kumbukumbu hizo
e) Masuala mapya yaliyoadiliwa/masuala mapya( kulingana na ajenda za siku)
f) Masuala mengineyo
g) Hitimisho
   i) Sahihi, jina la mwenyekiti na tarehe
   ii) Sahihi, jina la katibu na tarehe

**b). Maudhui**

Mtahiniwa adhihirishe majadiliano yalivyofanywa na hatima ya mjadala huo- yaani uamuzi ulioafikiwa na wanachama kuhusu suala zima la ufufuzi na uhaishaji wa shughuli za michezo katika taasisi za elimu nchini.

**Zifuatazo ni baadhi ya hoja:**

i) Mikakati ya kutambua na kukuza talanta mashinani
ii) Mikakati ya kuwamotisha wa wanamichezo

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com

iii) Uteuzi wa wasimamizi/viongozi katika michezo mbalimbali
iv) Shughuli za urekebishaji wa muundo msingi-viwanja
v) Ufadhili wa shughuli za michezo
vi) Kuandaliwa kwa semina za uhamasisho kuhusu michezo katika magatuzi mbalimbali
vii) Mikakati ya kuzuia maenezi ya korona viwanjani
viii) Jinsi ya kukabiliana na visa vya kutumia muku miongoni mwa wanariadha na wanamichezo wengine
ix) Kuandaliwa kwa warsha za mafunzo kwa makocha na wasimamizi wa michezo mbalimbali
x) Upanuzi wa mawanda ya michezo kwa kujumuisha tasnia nyingine zisizokuwepo
xi) Ushiriki katika michezo ya ndani na nje ya nchi

**Tanbihi**

Hii ni kumbukumbu wala si ripoti, sharti maadiliano yadhihirike na uamuzi ulioafikiwa kuonyeshwa

**2. Vijana wamekuwa wakichelea kuhusika katika mchakato wa uchaguzi. Jadili vyanzo vya hali hii huku ukiwapendekezea vijana umuhimu wa kubadili msimamo huu.**

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com

- Mchakato itahusisha kujiandikisha kama wapiga kura na vilevile,kampeni,kuelimisha wapiga kura,kuwania viti na kupiga kura kwenyewe. Yaani vyanzo vya vijana kutohusika kabisa.

Vyanzo:

- Ukosefu wa Akira
- Wizi wa kura/ tetesi za wizi wa kura
- Ukosefu/uhaba wa pesa za kuwania viti
- Wazee kutawala hali mchakato mzima
- Uvivu/uzembe miongoni mwa vijana
- Vijana kutoelewa umuhimu wa kuhusika
- Uhaba wa elimu miongoni mwa vijana/ uhaba wa elimu ya juu (shahada na kuendelea) itakayowawezesha kuwania viti.
- Mzozo ya uchaguzi/vita

HAKIKI MAJIBU

Umuhimu wa kubadili msimamo huu/umuhimu wa kuhusika katika mchakato wa uchaguzi/umuhimu wa uchaguzi

- Kuchagua viongozi bora/wenye maadili/kukabiliana na uongozi mbaya
- Kupata maendelea kama vili muundo msingi iletwayo na uongozi bora

- Kupata kuchagulia kuwa viongozi na kuhusika katika maamuzi muhimu nchini/kuamua mustakabali wao
- Kuelimisha wapiga kura kuhusu umuhimu wa uchaguzi
- Kupata nafasi za ajira
- Kuepuka vita vya baada ya uchaguzi/kutumiwa vibaya na wanasiasa

HAKIKI MAJIBU

3. **Tunga Kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo: Achanikaye kwenye mpini hafi njaa.**

Hii ni insha ya methali
Mtahiniwa abuni kisa kitakachodhihirisha maana ifuatayo:

a. Anayechoka akifanya kazi kwa jembe shambani hakosi chakula
b. Ataabikaye akifanya kazi ijapokuwa ngumu hatimaye atafaidika kwa kuwa kazi hiyo itamnufaisha au itamridhisha.

Matumizi ya methali hii.

i. Hutumiwa kumtia moyo mtu afanye kazi kwa bidii ili afanikiwe
ii. Hupigiwa mfano mtu aliyetaabika akitafuta hadi mwishowe akafanikiwa na pengine hata kupata maendeleo makuu
iii. Methali inaweza kutumiwa katika muktadha ifuatayo; mkulima anayefanya bidii, mwanafunzi anayejitahidi masomoni mwishowe afaulu, mwanasiasa anayefanya kampeni kwa bidii hadi akateuliwa na kadhalika

Mtahini anastahili kutunga insha ya masimulizi inayodhihirisha maana na matumizi ya methali hii.
Mtahini aonyeshe sehemu mbili ya methali
Mapambo ya lugha yawepo
Mwongozo wa kudumu urejelewe katika utuzaji.

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com

4. **Andika insha itakayomalizikia kwa:**

**…nilipotua nchini, nilishusha pumzi, nikamshukuru Jalia kwa kuponea chupuchupu katika uvamizi huo.**

- Hii ni insha ya mdokezo
- Mtahiniwa sharti amalizie kisa kwa maneno haya.
- Mtahiniwa atumie mbinu rejeshi ili kumrejesha msomaji kwenye matukio ya awali
- Mtahiniwa akiacha au aongeze neno moja au mawili atakuwa amejibu swali ila lichukuliwe kama kosa dogo tu la kimtindo
- Akikosa kuanza kwa mdokezo aliopewa atakuwa amejitungia swali **D- 02/20**

- Mtahiniwa aandike kichwa cha insha ingawa asipoandika si huja.

**Taswira zifuatazo zinaweza kuzingatiwa;**

i) Kisa kisimuliwe kuhusu mhusika ambaye anarejea nchini kutoka nje
ii) Mhusika huyu yumkini alikuwa ameenda ngambo kwa shughuli za kimasomo,kikazi au ziara
iii) Asimulie matukio yaliyofanyika katika nchi alikokuwa kiasi yeye kukushurtika kurejea nyumbani
iv) Anaweza kusimulia kuhusu uvamizi wa nchi moja dhidi ya nyingine kama ule wa Urusi dhidi ya Ukraine ambapo wageni wanakimbilia usalama
v) Yumkini mhusika huyu alikuwa akisafiri kurejea nyumbani baada ya kipindi cha masomo, ziara au kikazi kupitia cnhi fulani ambapo mashambulizi yanachipuka

- Usahihishaji wa insha ukadiriwe kulingana na viwango vya usahihishaji.
- Mtahiniwa asiondolewe alama za urefu badala yake mwongozo ufuatao wa kudumu uzingatiwe

| | |
|---|---|
| **Robo maneno** | **174** |
| **Nusu maneno** | **175 hadi 274** |
| **Robo tatu** | **275 hadi 374** |
| **Kamili** | **375 na zaidi.** |

**Tanbihi:**

Utahini ufanywe kwa kuzingatia mwongozo wa kudumu wa usahihishaji wa insha Kitaifa

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com